

Chuo Kikuu cha Al-Azhar
Kitivo cha Lugha na Ukalimani
Kitengo cha Lugha za Kiafrika

**Tofauti za Vitamkwa baina ya Kiswahili cha
Unguja na Kiswahili cha Tanzania Bara**

Dkt. Sameh Anwar Ibrahim Bayoumi

Kitengo cha Lugha za Kiafrika

Kitivo cha Lugha na Ukalimani

Chuo Kikuu cha Al-Azhar

Kairo

2018

ملخص البحث

اتسعت المنطقة السواحلية بفعل عوامل متعددة منها عوامل تاريخية وحضارية وجغرافية وتجارية ... إلخ. نتج عن ذلك تعدد لهجات المتحدثين بهذه اللغة. وتعد الاختلافات الصوتية من مظاهر الاختلاف المهمة بين لهجات اللغة السواحلية، من ثم اهتم هذا البحث بالوقوف على الاختلافات الصوتية بين لهجتي **Kibara** و **Kiunguja**.

جمع الباحث مادة هذا البحث عن طريقين؛ الأولى: هي التدوين، حيث قام الباحث بجمع مادته عن طريق الحوار المباشر مع أهل اللهجتين. والثانية: جمع الكلمات التي حدث لها اختلاف صوتي من معجمي Kamusi la Kamusi ya Kiswahili Sanifu و Kiswahili Fasaha.

رصد هذا البحث الاختلاف الصوتي بين لهجتي Kibara و Kiunguja، بهدف تحديد الاستخدام المختلف للصومات والصوات وأشباه الصوات. ليسهم بذلك في مكتبة اللغويات السواحلية ولهجاتها. واستخدم الباحث في سبيل ذلك منهج علم اللغة المقارن.

انقسم البحث إلى ثلاثة مباحث، مهد لها الباحث بمقدمة عن معايرة اللغة السواحلية؛ ناقش في المبحث الأول ظاهرة اختلاف الصومات، فعرض ظاهرة إبدال بعض الصومات في وسط الكلمة وفي بدايتها، ثم إقحام الصومات في وسط الكلمة وفي بدايتها، بعد ذلك ظاهرة حذف الصومات في وسط الكلمة وفي بدايتها، وفي النهاية قدم ظاهرة إبدال صامت بصائب. نفس الأمر قدمه الباحث في ظاهرة إبدال الصوات وإقحامها وحذفها وإطالتها في بداية الكلمات ووسطها ونهايتها. أما المبحث الثالث فقد خصه الباحث بقضية اختلافات أشباه الصوات في الكلمات وموقعها في الكلمة. وفي نهاية البحث قدم نتائج البحث وتوصياته. ثم ملحق البحث والمراجع التي اعتمد عليها.

Abstract

The Swahili region was expanded due to several factors, including historical, cultural, geographical and commercial ones. This resulted in a variety of dialects of Swahili speakers. The aspect of phonetic differences is very important among Swahili dialects, so this research is focusing on the vocal differences between the dialects of Kiunguja and .Kibara

The researcher collected the material of this research from two ways. **First:** through blogging, where the researcher collected his material through direct dialogue with the people of the two dialects. **Second:** through collecting words that have vocal differences from the lexicons “**Kamusi ya Kiswahili Sanifu**” and “**Kamusi la Kiswahili Fasaha**”.

This research is focusing on the vocal differences between the dialects of Kiunguja and Kibara, with the aim of determining the different usage of the silent, sounds and semi-sounds. By this way, the research contributes to the Library of Swahili Linguistics and its dialects. The researcher used a comparative linguistics approach. The research is divided into three sections that are mentioned in the introduction on the variety of the Swahili language. The first section outlines the phenomenon of the difference of the silent letters, the phenomenon of replacing some of the silent letters in the center and the beginning of the word, the phenomenon of inserting the silent in the center and the beginning of the word, then the phenomenon of deleting the silent in the center, and finally the phenomenon of replacing a silent with a vocal letter.

The same thing was presented by the researcher in the phenomenon of replacing the sounds and their combination, deleting and prolonging them at the beginning, center and end of the words. The third topic focused on the issue of semi-sound differences in words and its location in the word. At the end of the research, the researcher presented the research findings and recommendations. Then the research supplements and references relied on.

Utangulizi

Wazungumzaji wa Kiswahili wanatofautiana katika uzungumzaji wao kutoka eneo moja na jengine, tofauti hizo zimetokana na tofauti za kilahaja. Ingawa wazungumzaji wa lahaja tofauti za lugha moja wanatofautiana kimatamshi na pia katika baadhi ya msamiati na maana zake ila wazungumzaji hao wanaweza kuelewana.

Mtafiti aliishi muda mrefu Tanzania takriban miaka minne na nusu Zanzibar na miaka miwili Dar es Salaam, ambapo aliona tofauti za kimatamshi baina ya Kiswahili cha Tanzania Bara na Kiswahili cha Zanzibar.

Mswahili wa Bara anasema akimkaribisha mgeni: ‘kalibu Dar’ na Mswahili wa Unguja husema: ‘karibu Zanzibar’. “Mswahili wa Bara husema ‘tini’, ‘kitwa’ na ‘ndia’ badala ya maneno ya Zanzibar ‘chini’, ‘kichwa’ na ‘njia’ na kwa nadra hutumia neno tofauti, kwa mfano, ‘kuketi’ badala ya ‘kukaa’. Lakini katika mazungumzo, tofauti ni ndogo sana na hazitatizi mtu ila katika mara ya kwanza”⁽¹⁾. Isipokuwa tofauti baina ya Kiswahili cha Bara na Kiswahili cha Unguja hazipatikani tu katika vitamkwa, aidha zinaweza kupatikana katika silabi⁽²⁾ ambapo Mswahili wa Bara husema ‘sisi’, ‘sihi’, ‘chacharika au chakarika’, na Mswahili wa Unguja anaweza kusema: ‘sisi au siye’, ‘sihi au nasihi’, ‘chacharika’ n.k.

Hivyo, mtafiti akaanza kukusanya baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo wazungumzaji wa Bara wanatamka kwa njia tofauti na wazungumzaji wa Zanzibar, kisha kaanza utafiti huu uliochunguza tofauti za vitamkwa baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Tanzania Bara.

Mwanzoni mtafiti aliquwa na wazo kuwa lahaja ya Kibara ndiyo ambayo ina mpishano wa konsonanti **I : r**, pamoja na tofauti nyingine za vitamkwa. Lakini baada ya kuchunguza suala hili na kuanza kusajili baadhi ya maneno yanayotamkwa tofauti, akagundua kuwa si Kibara

(1) MBAABU, Ireri: **Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili**, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 2007, uk. 16.

(2) Mtafiti amekusanya tofauti zilizo baina ya Kiswahili cha Bara na Kiswahili cha Unguja katika silabi, lakini hajazizungumzia katika utafiti huu na atazichunguza katika utafiti mwengine.

peke yake ambacho wazungumzaji wake hutamka baadhi maneno yake kwa njia mbadala.

Hapo mtafiti aliweka baadhi ya maswali ili ajilazimike kuyajibu, mionganoni mwa maswali hayo ni pamoja na:

1. Lahaja gani atazishughulikia?
2. Nyanja gani za Kiismu ataichunguza?

Hapo mtafiti aliamua kuchagua lahaja mbili nazo ni Kiunguja kwa upande wa Zanzibar na Kibara kwa upande wa Tanzania Bara kwani mtafiti aliwahi kuishi Zanzibar na Dar es Salaam. Kuhusu nyanja za uchunguzi huu, basi mtafiti aliamua kuchunguza tofauti za vitamkwa baina ya lahaja hizo mbili.

Baada ya hapo mtafiti alitayarisha baadhi ya maswali mengine kabla ya kuanza uchunguzi wake, mionganoni mwa maswali hayo ni:

1. Je, Lahaja ya Kiunguja ina mpishano wa konsonanti **l : r** ?
2. Tofauti za konsonanti zinatokea zaidi katika lahaja ipi?
3. Tofauti za irabu zinatokea zaidi katika lahaja ipi?
4. Mpishano wa konsonanti unatokea zaidi mwanzoni mwa neno au katikati yake?
5. Mpishano wa irabu unatokea zaidi mwanzoni mwa neno, katikati yake, au mwishowe?
6. Udondoshaji wa vitamkwa hutokea zaidi katika lahaja ipi?
7. Urefushaji wa irabu unatokea zaidi katika lahaja ipi?
8. Upachikaji wa irabu unatokea zaidi katika lahaja ipi na kwa vitamkwa gani?

Data ya utafiti huu umekusanywa kwa kutumia mbinu mbili:

Ya kwanza: mbini za usaili na hojaji, ambapo mtafiti alikusanya data akiwa ana kwa ana na wazungumzaji.

Ya pili: mbinu ya kukusanya data kutoka kwa kamusi mbili; kamusi ya Kiswahili Sanifu⁽¹⁾ na Kamusi la Kiswahili Fasaha⁽²⁾, nayo ni mbinu iliyotumika kwa kiwango kikubwa zaidi kwani ndiyo iliyompa mtafiti

(1) **TUKI: Kamusi ya Kiswahili Sanifu**, Oxford University Press, East African Ltd, Toleo la tatu, 2014.

(2) **BAKIZA: Kamusi la Kiswahili Fasaha**, Oxford University Press, East African Ltd, chapa ya kwanza, 2010.

fursa kubwa ya kukusanya tofauti za vitamkwa zilizopo baina ya lahaja mbili ambazo zilifika 442, ambapo mtafiti alizainisha katika tofauti za matumizi ya konsonanti, tofauti za matumizi ya irabu na tofauti za matumizi ya viyeyusho.

Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umebainisha kuwa kuna tofauti zisizo chache za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara, na uchunguzi zaidi unahitajika kuchanguza chanzo na sababu za tofauti hizo.

Utafiti huu umebainisha na kujadili yafuatayo:

1. Tofauti za konsonanti zilizopo baina ya Kiunguja na Kibara.
2. Tofauti za irabu zilizopo baina ya Kiunguja na Kibara.
3. Tofauti za viyeyusho zilizopo baina ya Kiunguja na Kibara.

Tatizo la Utafiti

Kama tujuavyo, kuna tafiti chache zilizokwishafanywa kuchunguza tofauti za usemajji wa lugha ya Kiswahili au lahaja za Kiswahili zitumikazo katika maeneo tofauti, zile tafiti zinazobainisha kuwa kuna tofauti za kimatamshi kutoka eneo moja hadi jingine, isipokuwa mtafiti hajawahi kusikia kuwa kuna utafiti hata mmoja uliofanywa katika tofauti za vitamkwa baina ya Kiswahili kizungumzwacho maeneo ya Dar es Salaam na Pwani kule Tanzania Bara na Kiswahili kizungumzwacho Unguja.

Basi kutokana na sababu hiyo, utafiti huu umejaribu kuchunguza kwa kina tofauti za vitamkwa katika Kiswahili cha Unguja na cha Bara.

Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umejielekeza katika kujibu maswali yafuatayo:

- (a) Kuna tofauti gani za konsonanti zinazojibainisha baina ya Kiunguja na Kibara?
- (b) Kuna tofauti gani za irabu zinazojidhihirisha baina ya Kiunguja na Kibara?
- (c) Kuna tofauti gani za viyeyusho zilizopo baina ya Kiunguja na Kibara?

Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika mgawanyo wa lahaja na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Umuhimu wa utafiti huu unajibainisha katika yafuatayo:

- (a) Utafiti huu umechunguza kwa kina vipengele muhimu vinavyobainisha tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara.
- (b) Utafiti huu ni mwongozo na msaada kwa watafiti na wanafunzi watakaofanya tafiti zaidi kuhusu tofauti za vitamkwa na usemajji wa lugha ya Kiswahili katika Unguja na maeneo mengine.
- (c) Utafiti huu ni rejeo muhimu katika kuchangia taaluma ya isimu ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake.

Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimaelezo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielezo cha kuelezea jambo. Kiunzi cha nadharia ambacho kilitumika katika utafiti huu ni nadharia ya Isimulinganishi. Isimulinganishi ni tawi la Isimuhistoria linalojishughulisha na ulinganishaji wa lugha ili kuanzisha uhusiano wake wa kihistoria. Kiunzi hiki cha kinadharia kinachunguza lugha tofauti zenye uhusiano na asili moja hali kadhalika lahaja tofauti ya lugha moja.

Utafiti huu ultumia muundo wa kimaelezo katika kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Data zilipangwa kutokana na makundi yanayolingana.

Data zilizokusanywa katika utafiti huu, zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na majedwali kwa uchambuzi wa kihesabu. Data ambazo zilichambuliwa kwa njia ya majedwali pia zilifanuliwa kwa kuwekwa maelezo.

Usanifishaji wa Kiswahili

Otografia ya Kiswahili ilikuwa inabadilika mara kwa mara kwa muda mrefu mpaka ikatulia kwa sura iliyotumika siku hizi. Mdee

alitaja namna za mabadiliko ya otografia ya maneno ya Kiswahili kuanzia 1870 mpaka 1939⁽¹⁾ kama yafuatayo:

Steere (1870)	Krapf (1882)	Nettelbladt (1891)	Madan (1903)	Sacleux (1939)	Current Spelling
<i>afathali</i>	<i>afathali</i>	<i>afasali</i>	<i>afathali</i>	<i>afazali / afuzali / afzali</i>	<i>afadhali</i>
<i>afya</i>	<i>afia / afya</i>	<i>afia</i>	<i>afia / afya</i>	<i>Afyा</i>	<i>afya</i>
<i>assubui / ussubui</i>	<i>assubukhi / ussubukhi / essubukhi</i>	<i>assubui / ussubui</i>	<i>assubuhi / subuhi / ussubui</i>	<i>asubuhi / ussubuhi</i>	<i>asubuhi</i>
<i>athuuri</i>	-	<i>asuuri</i>	<i>athuuri</i>	<i>azuhuri / aduhuri</i>	<i>adhuuri</i>
<i>burre</i>	<i>burre</i>	<i>bure</i>	<i>burre</i>	<i>bure</i>	<i>bure</i>

Mwenye kuangalia maneno yaliyotajwa hapo juu katika jedwali, anaweza kugundua kuwa maneno hayo ni maneno mkopo; maana maneno yaliyoingia katika Kiswahili yalichukua muda mpaka yakatoholewa na kutumika kama yalivyo hivi sasa. Kadhalika Mdee aliandika: “Compare also the spelling of words in their current orthography in brackets: In Velten (1903), *muungu* (mungu), *maradi* (maradhi), *qabla* (kabla), *tawalli* (tawala), *qissa* (kisa), *radi* (radhi), *afadali* (afadhali), *zayidi* (zaidi), *assubuhi* (asubuhi), *el-jumaa* (ijumaa), *barza* (baraza), *chinsha* (chinja), *billa* (bila), and in Seidel (1941), *mudda* (muda), *fezza* (fedha), *ruddisha* (rudisha), *waqati* (wakati), *qasirika* (kasirika), *soqo* (soko), *gora* (jora), *boonde* (bonde), *qoodi* (kodi), *nakhodha* (nahodha)⁽²⁾.

Hapo tunaweza kuona kuwa neno ‘maradi’ baada ya kutohelewa likawa ‘maradhi’, ‘el-jumaa’ likawa ‘Ijumaa’ kwa kuwa neno likafuata sarufu maumbo ya Kiswahili baada ya kutohelwa, ‘mudda’ likawa ‘muda’ kwani katika Kiswahili kawaida konsonanti haifuatani na konsonanti lazima iwepo irabu, neno ‘qabla’ likawa ‘kabla’ kwani herufi ‘q’ haipo tena katika Kiswahili cha kisasa baada ya kuandikwa kwa herufi za Kirumi, hali kadhalika neno ‘nakhodha’ likawa

(1) Mdee, James S.: **Dictionaries and the Standardization of Spelling in Swahili**, Institute for Kiswahili Research, University of Dar es Salaam, Tanzania, <http://lexikos.journals.ac.za>, p. 123.

(2) Nukuu iliyopita, uk. 123.

‘nahodha’ kwa kuwa herufi ‘kh’ haipatikani sana katika Kiswahili cha kisasa, aidha neno ‘boonde’ likawa ‘bonde’ ingawa ni neno asili la Kiswahili ila herfu ‘o’ ikadondoshwa ili kurahisisha kulitamka.

Hayo yanamaanisha kuwa lugha ya Kiswahili na maneno yake ilichukua muda mrefu sana mpaka ikawa kama tunavyoisikia siku hizi. Hapa lazima tuashirie masuala mawili:

Suala la kwanza: hayo yametokea kwa Kiunguja kwani Krapf na wenzake walishughulikia na Kiunguja zaidi ya lahaja nyingine mpaka wakatunga kamusi kwa lahaja hiyo ya Kiunguja.

La pili: Kiswahili kilikuwa kinatumika kabla ya Steere (1870) na maneno yake pia yalikuwa yanatofautiana katika otografia yake lakini kabla ya Steere kulikuwa hamna tafiti za kina za kusajili na kudhihirisha tofauti hizi katika otografia ya Kiswahili na lahaja zake.

Hata hivyo, michakato na harakati nyingine zilifanyika katika kusanifisha Kiswahili ambapo “wakati wa mkutano wa mwaka wa 1928 mjini Mombasa mambo kadha yalikisaidia Kiunguja. Kwanza, ni mkutano wa Dar es Salaam wa mwaka 1925 ambapo Tanganyika na Zanzibar zilikichagua Kiunguja kuwa Kiswahili sanifu. Maendeleo ya maandishi yaliyokubaliwa mwaka huo 1925, yalikuwa karibu sawa na yale ya U.M.C.A. wakati huo karibu vitabu vyote vya misheni vilitoka Zanzibar na tayari kulikuwa na kitabu cha Steere *A Handbook of the Swahili Language* ambacho kilikuwa kielelezo cha kuigwa kimaandishi”⁽¹⁾.

Ireri MBAABU alisema “Kiswahili cha Bara kinachozungumziwa na Murison kinafanana na Kimvita. ambapo anataja lahaja sita (badala ya saba alizokusudia), ambazo anadai ndizo Kiswahili safi na sawa, ni tatu tu zilizo na umuhimu huo; nazo ni Kiunguja, Kimvita na Kiamu. kufikia mwaka 1928, ambapo lahaja ya usanifishaji ilikuwa imekwishajadiliwa kikamilifu, ni Kiunguja na Kimvita tu zilizokuwa zina nafasi kubwa ya kuchaguliwa hasa kwa sababu ya utafiti uliofanyiwa lahaja hizo mbili”⁽²⁾.

Usanifishaji wa Kiunguja kuwa ni lahaja sanifu unarudi Januari 1930 “ambapo serikali za kikoloni za Kenye, Uganda, Tanganyika na

(1) MBAABU, uk. 19.

(2) NUKUU ILYOPITA, uk. 17.

Unguja ziliunda kamati ya kimataifa ya Kiswahili. Kamati hii ilipewa wajibu wa kusanifisha maendelezo na sarufi ya Kiswahili kwa kutumia lahaja ya Kiunguja”⁽¹⁾.

Utafiti huu unashughulikia lahaja mbili; Kiunguja kinachotumika Zanzibar mjini⁽²⁾ na Kiswahili cha Bara kinachozungumziwa Dar es Salaam na maneno ya Pwani. “Mabaraza na vyombo wenza vya kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa upande wa Tanzania Bara na yale ya Tanzania Zanzibar hivi karibuni yameidhinisha kamusi za Kiswahili zinazopelekea kuwa na vielelezo anuwai vya usanifu wa lugha ya Kiswahili. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS) ya TUKI (sasa TATAKI) ya 2004 na ile ya Kamusi la Kiswahili Fasaha (KKF) ya BAKIZA ya 2010 ni ushahidi kuwa launi za Kiswahili Sanifu dhidi ya Kiswahili Fasaha zinarasimishwa. Kwa kutumia vigezo vya nadharia ya usanifishaji lugha ya Haugen (1966, 1987), makala haya yanajenga hoja kuwa tayari tumeshapata launi rasmi mbili za Kiswahili”⁽³⁾. Basi “Uchunguzi wa kina wa kamusi hizo unadhihirisha tofauti za msingi katika vigezo mbalimbali vya kiisimu na kimatumizi vinavyothibitisha tofauti rasmi za launi tutakazoziita Sanifu na Fasaha”⁽⁴⁾.

(1) Mbaabu, uk. vi.

(2) Pengine huitwa Kimji

(3) Kipacha, Ahmad: **Launi za Kiswahili Sanifu na Kiswahili Fasaha kwa Tanzania Bara na Zanzibar**, SWAHILI FORUM 19 , 2012, uk. 1.

(4) Nukuu iliyopita, uk.2.

Sehemu ya Kwanza

Tofauti za Konsonanti

Hapa mtafiti alijaribu kuchunguza tofauti zilizopo baina ya aina mojawapo za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti ambazo ni sauti zitamkazo “kwa kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni kwenda nje ukipitia ama chemba ya kinywa au chemba ya pua”⁽¹⁾.

A. Mpishano wa Konsonanti:

Tofauti za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti baina ya Kiunguja na Kibara zilitokea katika maneno 112 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Mpishano wa Konsonanti katikati ya Neno:

Kuna tofauti za vitamkwa baina Kiunguja na Kibara zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti katikati ya neno. Mpishano wa aina hii umetokea katika maneno 62 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Konsonanti I : r

Kibara	Kiunguja
dalji	darji
dandalo	dandaro
filimbi	firimbi
gudulia	guduria
ulimbo	urimbo

Hapa tunaona mpishano wa konsonanti I : r katikati ya neno, nao umetokea mara 14 katika mada ya utafiti, mionganini mwao ni mifani ya hapo juu.

(1) Massamba, David P. B & Y.M., Kihore & Y. P., Msanjila: **Fonolojia ya Kiswahili Sanifu**, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, chapa ya tatu, 2013, uk. 90.

- Konsonanti **h : kh**

Kibara	Kiunguja
bah <u>ili</u>	bak <u>hili</u>
bu <u>heri</u>	buk <u>heri</u>
joh <u>o</u>	jok <u>ho</u>
taah <u>ira</u>	taak <u>hira</u>

Tunaona hapa mpishano wa konsonanti **h : kh** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno manane, miongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Konsonanti **r : l**

Kibara	Kiunguja
bir <u>ingani</u>	bil <u>ingani</u>
cher <u>ewa</u>	che <u>lewa</u>

Hapa tunaona mpishano wa konsonanti **r : l** katikati ya neno, nao umetokea mara 3, miongoni mwao ni mifani ya hapo juu.

Aidha kuna tofauti nyingine za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara mbili mbili katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **g : j**

Kibara	Kiunguja
changa	chanja ⁽¹⁾
ugea	ujea

- Konsonanti **n : l**

Kibara	Kiunguja
sa <u>namaki</u>	sa <u>lamaki</u>
segem <u>nege</u>	segem <u>lega</u>

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **b : v**

(1) Asili ya neno ni “changa”, ila linaweza kutumika katika Kiunguja “chanja”.
Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 43.

Kibara	Kiunguja
chambi	cham <u>y</u> i
• Konsonanti d : g	
Kibara	Kiunguja
tund <u>ika</u>	tungika
• Konsonanti g : k	
Kibara	Kiunguja
chanjagaa	chanjak <u>aa</u>
• Konsonanti j : d	
Kibara	Kiunguja
bajia	bad <u>ia</u>
• Konsonanti l : h	
Kibara	Kiunguja
selelea	sehe <u>lea</u>
• Konsonanti p : k	
Kibara	Kiunguja
nyopoa	nyok <u>oa</u>
• Konsonanti r : d	
Kibara	Kiunguja
chu <u>ruza</u>	chudu <u>za</u>
• Konsonanti r : z	
Kibara	Kiunguja
chiririka	chiriz <u>ika</u>
• Konsonanti s : t	
Kibara	Kiunguja
wewe <u>seka</u>	wewet <u>eka</u>
• Konsonanti sh : ch	
Kibara	Kiunguja

pensheni

pencheni

- Konsonanti **t : r**

Kibara
papatika

Kiunguja
paparika

- Konsonanti **z : dh**

Kibara
izara

Kiunguja
idhara

- Konsonanti **z : k**

Kibara
chokomeza

Kiunguja
chochomeka

- Konsonanti **z : r**

Kibara
gwaza

Kiunguja
gwara

Kiswahili cha Bara

- Konsonanti **r : l**

Kiunguja
arijojo
achari

Kibara
alijojo
achali

Tunaona hapa mpishano wa konsonanti **r : l** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno manne mi^ongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Konsonanti **h : kh**

Kiunguja
akhirika
ubahkili

Kibara
ahirika
ubahili

Hapa tunaona mpishano wa konsonanti **h : kh** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno matatu mi^ongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa konsonanti katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **g : j**

Kiunguja
shemegi

Kibara
shemeji

- Konsonanti **g : k**

Kiunguja
tangi

Kibara
tanki

- Konsonanti **j : ch**

Kiunguja
ujukuti

Kibara
uchukuti

- Konsonanti **j : g**

Kiunguja
njorinjori

Kibara
ngoringori

- Konsonanti **k : s**

Kiunguja
alika

Kibara
alisa

- Konsonanti **l : r**

Kiunguja
foliti

Kibara
foriti

- Konsonanti **m : n**

Kiunguja
samsuri

Kibara
sansuri

- Konsonanti **r : t**

Kiunguja
burura

Kibara
buruta

- Konsonanti s : sh

Kiunguja
garasa

Kibara
garasha

- Konsonanti v : f

Kiunguja
uchovu

Kibara
uchofu

- Konsonanti z : d

Kiunguja
utenzi

Kibara
utendi

- Konsonanti z : s

Kiunguja
uumisi

Kibara
uumizi

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa tofauti za matumizi ya konsonanti katika Kiswahili cha Unguja katikati ya neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **l : r**. ama tofauti za matumizi ya konsonanti katika Kiswahili cha Bara katikati ya neno hutokea zaidi kwa mpishano wa vitamkwa **l : r** na **h : kh**

Hali kadhalika inabainika kuwa tofauti za matumizi ya konsonanti baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Bara hutokea zaidi katika mpishano wa konsonanti katikati ya neno.

2. Mpishano wa Konsonanti mwanzoni mwa Neno:

Kuna tofauti za vitamkwa baina Kiunguja na Kibara zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Mpishano wa aina hii umetokea mara 50 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Konsonanti h : kh

Kibara
halisi
heri

Kiunguja
khalisi
kheri

<u>hitima</u>	<u>khitima</u>
<u>hulka</u>	<u>khulka</u>
<u>humusi</u>	<u>khumusi</u>

Hapa tunaona mpishano wa vitamkwa **h** : **kh** mwanzoni mwa neno, nao umetokea mara 11 katika mada ya utafiti, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

- Konsonanti **l** : **d**

Kibara	Kiunguja
<u>lema</u>	<u>dema</u>
<u>limbuu</u>	<u>dimbuu</u>

Hapa tunaona tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara, tofauti hizo zimetokana na mpishano wa **l** : **d** mwanzoni mwa neno, ambapo idadi zake zilifikia 3, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo kuna tofauti nyingine za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara mbili mbili kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **g** : **j**

Kibara	Kiunguja
<u>goma</u>	<u>joma</u>
<u>gunda</u>	<u>junda</u>

- Konsonanti **g** : **k**

Kibara	Kiunguja
<u>gubigubi</u>	<u>kubi<u>k</u>ubi</u>
<u>gubika</u>	<u>kubi<u>k</u>ika</u>

- Konsonanti **h** : **ch**

Kibara	Kiunguja
<u>hama</u>	<u>chama</u>
<u>hamia</u>	<u>chamia</u>

- Konsonanti **l** : **r**

Kibara	Kiunguja
<u>legalega</u>	<u>regarega</u>
<u>lenga</u>	<u>renga</u>

- Konsonanti **s : sh**

Kibara <u>sanjari</u> <u>sindano</u>	Kiunguja <u>shanjari</u> <u>shindano</u> ⁽¹⁾
---	--

- Konsonanti **sh : ch**

Kibara <u>shanuo</u> <u>shunga</u>	Kiunguja <u>chanuo</u> <u>chunga</u>
---	---

Aidha kuna tofauti nyingine za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **b : v**

Kibara <u>biringa</u>	Kiunguja <u>viringa</u>
---------------------------------	-----------------------------------

- Konsonanti **ch : k**

Kibara <u>chobea</u>	Kiunguja <u>kobea</u>
--------------------------------	---------------------------------

- Konsonanti **f : v**

Kibara <u>fukuta</u>	Kiunguja <u>yukuta</u>
--------------------------------	----------------------------------

- Konsonanti **j : g**

Kibara <u>jiriwa</u>	Kiunguja <u>giriwa</u>
--------------------------------	----------------------------------

- Konsonanti **n : m**

Kibara <u>nchoro</u>	Kiunguja <u>mchoro</u>
--------------------------------	----------------------------------

(1) Asili ya neno ni “sindano” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “shindano” kwa maana ya “(1) kifaa chenye ncha kinachotumika kushonea vitu kwa kutumia uzi (2) kifaa kinachotumika kutilia dawa katika mwili wa mgonjwa”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 371.

- Konsonanti **p : ch**

Kibara	Kiunguja
<u>pagawa</u>	<u>chagawa</u>

- Konsonanti **v : b**

Kiunguja	Kibara
<u>bumburuka</u>	<u>yumburuka</u>

- Konsonanti **r : l**

Kibara	Kiunguja
<u>renga</u>	<u>lenga</u>

- Konsonanti **sh : s**

Kibara	Kiunguja
<u>shikio</u>	<u>sikio⁽¹⁾</u>

- Konsonanti **th : s**

Kibara	Kiunguja
<u>thubutu</u>	<u>subutu</u>

- Konsonanti **v : d**

Kibara	Kiunguja
<u>vumbi</u>	<u>dumbi</u>

- Konsonanti **v : f**

Kibara	Kiunguja
<u>vugaza</u>	<u>fugaza</u>

- Konsonanti **z : s**

Kibara	Kiunguja
<u>zaatari</u>	<u>saaturi</u>

Kiswahili cha Bara

(1) Asili ya neno ni “shikio” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “sikio”.
Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 364.

- Konsonanti **ch : t**

Kiunguja

chafi
chubwi

Kibara

tafi
tubwi

Hapa tunaona tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zilizotokana na mpishano wa konsonanti **ch : t** mwanzoni mwa neno. Mpishano wa aina hii umetokea mara 5.

- Konsonanti **l : r**

Kiunguja

randana
rodi

Kibara

landana
lodi

Tunaona hapa mpishano wa konsonanti **l : r** mwanzoni mwa neno, nao umetokea mara 3 katika mada ya utafiti.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **dh : d**

Kiunguja

dhumna

Kibara

dumna

- Konsonanti **j : ch**

Kiunguja

jagina

Kibara

chagina

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa tofauti za matumizi ya konsonanti katika Kiswahili cha Unguja mwanzoni mwa neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **h : kh**. Ama tofauti za matumizi ya konsonanti katika Kiswahili cha Bara hutokea zaidi mwanzoni mwa neno kwa mpishano wa **ch : t** na **l : r**.

B. Upachikaji wa Konsonanti:

Vile vile tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na upachikaji wa konsonanti ambapo kitamkwa kimoja

kinaweza kupachikwa mwanzoni mwa neno au katikati yake⁽¹⁾. Tofauti za aina hii zimetokea mara 19 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Upachikaji wa Konsonanti katikati ya Neno:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zilizosababishwa na upachikaji wa konsonanti katikati ya neno zimetokea mara 12 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Konsonanti **n**

Kiunguja	Kibara
<u>undugu</u>	udugu
timanzi ⁽²⁾	timazi

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa konsonanti **n** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno 3, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

- Konsonanti **r**

Kiunguja	Kibara
Pekura	pekuu
U <u>rowevu</u>	uowevu

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa konsonanti **r** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno 2.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na upachikaji wa konsonanti katikati ya neno, ambapo kila tofauti imetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **g**

Kiunguja	Kibara
gingiza	giniza

(1) Hapa lazima nitaje kuwa Kiunguja kwa mtafiti ni lahaja sanifu; maana ikitokea tofauti za vitamkwa baina yake na Kibara, basi utamkaji fasaha aghalabu ni wa Kiunguja.

(2) Asili ya neno ni “timazi” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “timanzi”.
Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 397.

- Konsonanti **m**

Kiunguja
nyamamfu

Kibara
nyamafu

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa upachikaji wa konsonanti katika Kiswahili cha Unguja katikati ya neno hutokea zaidi katika vitamkwa **n, r**.

Kiswahili cha Bara

- Konsonanti **r**

Kibara
serezi
tambara

Kiunguja
seezi
tambaa

Hapa tunaona tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa konsonanti **r** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno mawili.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **h**

Kibara
junaa

Kiunguja
junaha

- Konsonanti **m**

Kibara
buburusha

Kiunguja
bumburusha

- Konsonanti **n**

Kibara
enhee

Kiunguja
ehee

Kutokana na yaliyotangulia inabainika wazi kuwa upachikaji wa konsonanti katika Kiswahili cha Bara katikati ya neno hutokea zaidi katika kitamkwa **r**. Hali kadhalika upachikaji wa konsonanti hutokea zaidi katikati ya neno kuliko mwanzoni mwa neno.

Aidha upachikaji wa konsonanti katikati ya neno hutokea zaidi katika Kiunguja kuliko Kibara.

2. Upachikaji wa Konsonanti mwanzoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na upachikaji wa konsonanti mwanzoni mwa neno zimetokea mara 7 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

Upachikaji wa konsonanti mwanzoni mwa neno katika Kiunguja umejibainika katika vitamkwa vitatu mara mbili mbili kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **h**

Kiunguja	Kibara
<u>halizeti</u> ⁽¹⁾	alizet
<u>hamrawi</u>	amrawi

- Konsonanti **k**

Kiunguja	Kibara
<u>kosha</u> ⁽²⁾	osha
<u>kota</u>	ota

- Konsonanti **m**

Kiunguja	Kibara
<u>mwito</u> ⁽³⁾	wito
<u>mdele</u>	dele

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa upachikaji wa konsonanti katika Kiunguja mwanzoni mwa neno hutokea katika vitamkwa **h , k , m** .

(1) Asili ya neno ni “alizeti” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “halizeti”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 7.

(2) Asili ya neno ni “osha” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “kosha”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 316.

(3) Asili ya neno ni “wito” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “mwito”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 460.

Kiswahili cha Bara

- Konsonanti **m**

Kibara
mduara

Kiunguja
duara

Hapa tunaona tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa konsonanti **m** mwanzoni mwa neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa upachikaji wa konsonanti katika Kiswahili cha Bara unatokea katika kitamkwa **m**.

C. Udondoshaji wa Konsonanti:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na udondoshaji wa konsonanti, nao ni utaratibu wa kutoa kitamkwa. Tofauti za aina hii zimetokea mara 23 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo.

1. Udondoshaji wa Konsonanti katikati ya Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa konsonanti katikati ya neno zimetokea mara 11 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Konsonanti **n**

Kiunguja
nyogea
pogoo

Kibara
nyongea
pongoo

Hapa tunaona udondoshaji wa konsonanti **n** katikati ya neno, nao umetokea mara 2 katika mada ya utafiti.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **d**

Kiunguja
steni

Kibara
stendi

- Konsonanti **h**

Kiunguja
fii

Kibara
fihi

- Konsonanti **k**

Kiunguja
deua

Kibara
dekua

- Konsonanti **r**

Kiunguja
fuu

Kibara
furu

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa konsonanti katikati ya neno katika Kiunguja hutokea zaidi katika kitamkwa **n**.

Kiswahili cha Bara

- Konsonanti **l**

Kibara
turubai
ukengee

Kiunguja
turubali
ukengele

Hapa tunaona tofauti ya vitamkwa iliyosababishwa na udondoshaji wa konsonanti **l** katikati ya neno, nao umetokea mara 2.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa konsonanti katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **d**

Kibara
beni

Kiunguja
bendi

- Konsonanti **j**

Kibara
barai

Kiunguja
baraji

- Konsonanti **k**

Kibara	Kiunguja
pitua	<u>pituka</u>

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa konsonanti katikati ya neno katika Kiswahili cha Bara hutokea zaidi katika kitamkwa **l**.

2. Udondoshaji wa Konsonanti mwanzoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa konsonanti mwanzoni mwa neno zimetokea mara 10 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Konsonanti **h**

Kiunguja	Kibara
emkwa	<u>hemkwa</u>
iliki	<u>hiliki</u>

Hapa tunaona udondoshaji wa konsonanti **h** mwanzoni mwa neno, nao umetokea katika maneno matano, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Konsonanti **d**

Kiunguja	Kibara
ago	<u>dago</u>

- Konsonanti **sh**

Kiunguja	Kibara
ikiza ⁽¹⁾	<u>shikiza</u>

(1) Asili ya neno ni “shikiza” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “ikiza”.
Tazama: **Kamasi la Kiswahili Fasaha**, uk. 364.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa konsonanti mwanzoni mwa neno katika Kiunguja hutokea zaidi katika kitamkwa **h** .

Kiswahili cha Bara

- Konsonanti **h**

Kibara	Kiunguja
ebu	<u>hebu</u>
aidini	<u>haidini</u>

Hapa tunaona udondoshaji wa konsonanti **h** mwanzoni mwa neno, nao umetokea katika maneno mawili.

- Konsonanti **m**

Kibara	Kiunguja
dungudungu	<u>mdungudungu</u>

Hapa unaona udondoshaji wa konsonanti **m** mwanzoni mwa neno, nao umetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa konsonanti mwanzoni mwa neno katika Kiswahili cha Bara hutokea zaidi katika kitamkwa **h** .

3. Mpishano wa Konsonanti na Irabu katikati ya Neno:

Kuna tofauti nyingine za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinazosababishwa na ubadilishaji wa konsonanti kwa irabu katikati ya neno. Tofauti hizo zimetokea mara 2 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Bara

- (**n : a**)

Kibara	Kiunguja
ta <u>a</u> zia	<u>tan</u> zia

- (**z : o**)

Kibara	Kiunguja
be <u>u</u> o	<u>be</u> zo

Sehemu ya Pili

Tofauti za Irabu

Irabu ni “aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa pasi na kuwepo kizuizi chochote katika mkondohewa utokao mapafuni ukipitia chemba ya kinywa na chemba ya pua”⁽¹⁾.

Aidha tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na irabu kwa kuwepo aina mojawapo ya mpishano wa irabu, upachikaji, udondoshaji na urefushaji wa irabu.

A. Mpishano wa Irabu:

Tofauti za vitamkwa zinazosababishwa na mpishano wa irabu baina ya Kiunguja na Kibara zilitokea mara 153 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Mpishano wa Irabu katikati ya Neno:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zilizosababishwa na mpishano wa irabu katikati ya neno zimetokea mara 99 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu e : a

Kibara	Kiunguja
<u>j</u> emadari	<u>j</u> amadari
<u>j</u> eraha	<u>j</u> araha
<u>r</u> ekebisha	<u>r</u> akabisha
<u>s</u> eremala	<u>s</u> aramala
<u>z</u> eutuni	<u>z</u> aituni

Tunaona hapa mpishano wa irabu e : a katikati ya neno, nao umetokea mara 12, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

(1) Massaba & Kihore & Msanjila, uk. 24.

- Irabu e : i

Kibara	Kiunguja
bakteria	baktiria
debwani	dibwani
hekima	hikima
heshima	hishima
serikali	sirikali

Tunaona hapa mpishano wa irabu e : i katikati ya neno, nao umetokea mara 11, mionganini mifano ya hapo juu.

- Irabu a : e

Kibara	Kiunguja
tangua	tengua
bilashi	bileshi
hansa	hensa
saruni	seruni

Tunaona hapa mpishano wa irabu a : e katikati ya neno, nao umetokea mara 8, mionganini mifano ya hapo juu.

- Irabu i : u

Kibara	Kiunguja
bilula	bulula
fidua	fudua
simile	sumile

Tunaona hapa mpishano wa irabu i : u katikati ya neno, nao umetokea mara 6, mionganini mifano ya hapo juu.

- Irabu u : i

Kibara	Kiunguja
fukundi	fukindi
shubiri	shibiri
sufuri	sifuri

Tunaona hapa mpishano wa irabu u : i katikati ya neno, nao umetokea mara 5, mionganini mifano ya hapo juu.

Aidha kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara nne nne katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu **o : u**

Kibara	Kiunguja
ny <u>ofoa</u>	ny <u>ofua</u>
sok <u>oa</u>	suk <u>ua</u>

- Irabu **i : e**

Kibara	Kiunguja
b <u>inua</u>	benua
f <u>idhuli</u>	f <u>edhuli</u>

- Irabu **u : a**

Kibara	Kiunguja
ch <u>upia</u>	chap <u>ia</u>
d <u>uwaa</u>	d <u>awaa</u>

- Irabu **u : o**

Kibara	Kiunguja
b <u>urunga</u>	b <u>oronga</u>
p <u>unyeto</u>	p <u>onyeto</u>

Kuna tofauti nyingine imetokea mara 3 nayo ni:

- Irabu **a : i**

Kibara	Kiunguja
si <u>labasi</u>	si <u>libasi</u>
sta <u>hamili</u>	sta <u>himili</u>

Hali kadhalika, kuna tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara mbili mbili katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a : o**

Kibara	Kiunguja
ch <u>afuo</u>	cho <u>fuo</u>
f <u>akamia</u>	f <u>okomea</u>

- Irabu **a : u**

Kibara	Kiunguja
h <u>alkumu</u>	h <u>ulkumu</u>
s <u>aluti</u>	s <u>uluti</u>

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu **e : o**

Kibara	Kiunguja
ch <u>e</u> tezo	ch <u>otezo</u>

- Irabu **e : u**

Kibara	Kiunguja
fe <u>ruwili</u>	fu <u>ruwili</u>

- Irabu **i : a**

Kibara	Kiunguja
bi <u>skuti</u>	ba <u>skuti</u>

Kutokana na yaliyotajwa hapo juu, tunaweza kusema kuwa tofauti za matumizi ya irabu katika Kiswahili cha Unguja katikati ya neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **e : a , e : i** .

Kiswahili cha Bara

- Irabu **i : e**

Kiunguja	Kibara
gia	gea
oksijini	oksijeni
ri <u>kodi</u>	re <u>kodi</u>
ri <u>kodiplea</u>	re <u>codiplea</u>

Tunaona hapa mpishano wa irabu **i : e** katikati ya neno, nao umetoka mara 9, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Aidha kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetoka mara tatu tatu kwa namna ifuatayo:

- Irabu a : e

Kiunguja
thalathini
thamomita

Kibara
thelathini
themometa

- Irabu e : a

Kiunguja
breketi
penelti

Kibara
braketi
penalti

- Irabu i : u

Kiunguja
tipitipi
shifaa

Kibara
tupitupi
shifaa

- Irabu u : i

Kiunguja
udakuzi
furari

Kibara
udakizi
firari

Hali kadhalika, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara mbili mbili katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu u : o

Kiunguja
arubaini
tufaa

Kibara
arobaini
tofaa

- Irabu a : o

Kiunguja
wasia / usia
tafauti

Kibara
wasia / wosia
tofauti

- Irabu e : i

Kiunguja
aheri
ufedhuli

Kibara
ahiri
ufidhuli

Zaidi ya hayo, tofauti za aina hiyo zimetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu **i : o**

Kiunguja
thiolojia

Kibara
teoloujia

- Irabu **o : a**

Kiunguja
protokoli

Kibara
protokali

- Irabu **o : u**

Kiunguja
toasi

Kibara
tuasi

- Irabu **u : e**

Kiunguja
thuluthi

Kibara
theluthi

Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa tofauti za matumizi ya irabu katika Kiswahili cha Bara katikati ya neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **i : e**.

2. Mpishano wa Irabu mwishoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zilizosababishwa na mpishano wa irabu mwishoni mwa neno zimetokea mara 45 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu **o : u**

Kibara
chao
ng'ambo
ngano

Kiunguja
chau
ng'ambu
nganu

Tunaona hapa mpishano wa irabu **o : u** mwishoni mwa neno, nao umetokea mara 5, miiongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu **a : i**

Kibara	Kiunguja
dhamira <u>_</u>	dhamiri <u>_</u>
stata <u>_</u>	stati

Tunaona hapa mpishano wa irabu **a : i** mwishoni mwa neno, nao umetokea mara 4, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu **a : o**

Kibara	Kiunguja
dubwash <u>a</u>	dubwash <u>o</u>
posa <u>_</u>	poso

Tunaona hapa mpishano wa irabu **a : o** mwishoni mwa neno, nao umetokea mara 3, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

Aidha kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu mwishoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara mbili mbili kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a : e**

Kibara	Kiunguja
chan <u>a</u>	chan <u>e</u>
nuna <u>_</u>	nune

- Irabu **i : a**

Kibara	Kiunguja
jelezi <u>_</u>	jeleza <u>_</u>
sahali <u>_</u>	sahala <u>_</u>

- Irabu **i : u**

Kibara	Kiunguja
ghafuri <u>_</u>	ghafuru <u>_</u>
shababi	shababu

Hali kadhalika, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizotokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu **e : a**

Kibara
shibe

Kiunguja
shiba

- Irabu e : i

Kibara
chongoe

Kiunguja
chongoi

- Irabu o : i

Kibara
nduwaro

Kiunguja
nduwari

- Irabu u : a

Kibara
bereu

Kiunguja
berea

- Irabu u : i

Kibara
atomu

Kiunguja
atomi

- Irabu u : o

Kibara
tumbuu

Kiunguja
tumbuo

Kutokana na yaliyotangulia, inabainika wazi kuwa tofauti za matumizi ya irabu katika Kiswahili cha Unguja mwishoni mwa neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **o : u**.

Kiswahili cha Bara

- Irabu e : i

Kiunguja
shemere
tarawehé

Kibara
shemerí
tarawehí

Tunaona hapa mpishano wa irabu e : i mwishoni mwa neno, nao umetokea mara 3, miiongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu mwishoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara mbili mbili katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a : o**

Kiunguja
ndoanag
ukaangag

Kibara
ndoanog
ukaangog

- Irabu **i : a**

Kiunguja
tukwig
takbirig

Kibara
tukwag
takbirag

- Irabu **u : i**

Kiunguja
chemchemg
Israfilg

Kibara
chemchemg
Israfilig

- Irabu **u : o**

Kiunguja
barubarg
dafraug

Kibara
barobarog
dafraog

Aidha, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu mwishoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a : e**

Kiunguja
lembalemba

Kibara
lembelembea

- Irabu **a : i**

Kiunguja
istiwaag

Kibara
istiwaig

- Irabu **a : u**

Kiunguja
hamama

Kibara
hamamu

- Irabu **i : e**

Kiunguja
afandi

Kibara
afande

- Irabu **i : o**

Kiunguja
longitudi

Kibara
longitudo

- Irabu **i : u**

Kiunguja
ami

Kibara
amu

- Irabu **o : a**

Kiunguja
chavuo

Kibara
chavua

- Irabu **o : e**

Kiunguja
wicho

Kibara
wiche

- Irabu **o : u**

Kiunguja
lebo

Kibara
lebu

- Irabu **u : a**

Kiunguja
stimu

Kibara
stima

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa tofauti za matumizi ya irabu katika Kiswahili cha Bara mwishoni mwa neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **e : i**.

3. Mpishano wa Irabu mwanzoni mwa Neno:

Kuna tofauti za vitamkwa baina Kiunguja na Kibara zinazosababishwa na mpishano wa irabu mwanzoni mwa neno. Mpishano wa aina hii umetokea mara 9 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu **e : i**

Kibara	Kiunguja
<u>e</u> limika	<u>i</u> limika
<u>e</u> limu	<u>i</u> limu

Hapa tunaona mpishano wa irabu **e : i** mwanzoni mwa neno, nao umetokea mara 3, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na mpishano wa irabu mwanzoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a : e**

Kibara	Kiunguja
<u>a</u> pron	<u>e</u> pron

- Irabu **a : u**

Kibara	Kiunguja
<u>a</u> subuhi	<u>u</u> subuhi

- Irabu **e : o**

Kibara	Kiunguja
<u>e</u> haa	<u>o</u> haa

- Irabu **i : u**

Kibara	Kiunguja
<u>i</u> jara	<u>u</u> jira ⁽¹⁾

Basi ni wazi kuwa tofauti za matumizi ya irabu katika Kiswahili cha Unguja mwanzoni mwa neno aghalabu husababishwa na mpishano wa vitamkwa **e : i**.

(1) Asili ya neno ni “ijara” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “ujira”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 422.

Kiswahili cha Bara

- Irabu o : a

Kiunguja	Kibara
<u>ofisa</u>	<u>afisa</u>
<u>ofisi</u>	<u>afisi</u>

Tunaona hapa mpishano wa irabu **o : a** mwanzoni mwa neno, nao umetokea mara 2.

B. Upachikaji wa Irabu:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na upachikaji wa irabu mwanzoni, katikati na mwishoni mwake. Tofauti za aina hii zimetokea mara 49 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Upachikaji wa Irabu katikati ya Neno:

Tofauti za vitamkwa zinaweza kusababishwa na upachikaji wa irabu katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara 34 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu i

Kiunguja	Kibara
s <u>itahi</u>	stahi
bis <u>ibisi</u>	bisbisi
sh <u>itaka</u>	shtaka
sh <u>itaki</u>	shtaki
tak <u>rima</u>	takrima

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **i** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno kumi na nne, mionganini mwao mifano ya hapo juu.

- Irabu u

Kiunguja	Kibara
shar <u>uti</u>	sharti
bo <u>fulo</u>	boflo

shuwari

shwari

Hapa kuna tofauti nyingine ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **u** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno matano, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu a

Kiunguja
anka
talakini

Kibara
ankra
talkini

Aidha kuna tofauti nyingine ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **a** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno mawili.

- Irabu e

Kiunguja
ngoe

Kibara
ngoja

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **e** katikati ya neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia hapo juu, inabainika kuwa upachikaji wa irabu katika Kiswahili cha Unguja katikati ya neno hutokea zaidi katika kitamkwa **i** .

Kiswahili cha Bara

- Irabu i

Kibara
ariki
asikirimu
tashiwishi
pasipoti

Kiunguja
arki
askirimu
tashwishi
paspoti

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **i** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno tisa, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu a

Kibara

Kiunguja

aghalabu
takariri

aghlabu
takriri

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **a** katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno mawili.

- **Irabu u**

Kibara
ghafula

Kiunguja
ghafla

Aidha kuna tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **u** katikati ya neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa upachikaji wa irabu katika Kiswahili cha Bara katikati ya neno hutokeza zaidi katika kitamkwa **i**. Hali kadhalika tunaweza kusema kuwa upachikaji wa irabu hutokeza zaidi katikati ya neno kuliko mwanzoni na mwishoni mwa neno.

2. Upachikaji wa Irabu mwishoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na upachikaji wa irabu mwishoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara 11 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- **Irabu a**

Kiunguja
jiometria

Kibara
jiometri

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **a** mwishoni mwa neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

Kiswahili cha Bara

- **Irabu u**

Kibara
hafutaimu
ghalibu

Kiunguja
hafutaim
ghalib

taibu

taib

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **u** mwishoni mwa neno, nayo imetokea katika maneno saba, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu **i**

Kibara
halani
abadani

Kiunguja
halan
Abadan

Hapa kuna tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **i** mwishoni mwa neno, nayo imetokea katika maneno mawili.

- Irabu **a**

Kibara
entomolojia

Kiunguja
entomoloji

Aidha kuna tofauti nyingine ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **a** mwishoni mwa neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

3. Upachikaji wa Irabu mwanzoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na upachikaji wa irabu mwanzoni mwa neno zimetokea mara 4 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu **i**

Kiunguja
ihisani

Kibara
hisani

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **i** mwanzoni mwa neno, nayo imetokea katika neno moja tu.

Kiswahili cha Bara

- Irabu **u**

Kibara
uwayo
uweledi

Kiunguja
wayo
weledi

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa irabu **u** mwanzoni mwa neno, nayo imetokea katika maneno matatu, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

Kutokana na yaliyotangulia, inabainika kuwa upachikaji wa irabu katika Kiswahili cha Uguja mwanzoni mwa neno hutokea katika kitamkwa **i**. Ama upachikaji wa irabu katika Kiswahili cha Bara mwanzoni mwa neno, basi hutokea zaidi katika kitamkwa **u**.

C. Udondoshaji wa Irabu:

Kuna aina nyingine za tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara nayo ni udondoshaji wa irabu. Tofauti za aina hii zimetokea mara 42 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Udondoshaji wa Irabu katikati ya Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa irabu katikati ya neno zimetokea mara 28 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Uguja

- Irabu **i**

Kiunguja	Kibara
silka	<u>silika</u>
taklifu	<u>takilifu</u>
talbisi	<u>talibisi</u>

Hapa tunaona udondoshaji wa irabu **i** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno matano, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu **a**

Kiunguja	Kibara
hardali	<u>haradali</u>
darsa	<u>darasa</u>

Hapa tunaona udondoshaji wa irabu **a** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno 4, mionganini mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu **u**

Kiunguja	Kibara
-----------------	---------------

burdani	bur <u>u</u> dani
zuhra	zu <u>h</u> ura

Tunaona hapa udondoshaji wa irabu **u** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno 3, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu e

Kiunguja	Kibara
rehma	re <u>h</u> ema

Aidha kuna udondoshaji wa irabu **e** katikati ya neno, nao umetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa irabu katikati ya neno katika Kiswahili cha Unguja hutokea zaidi katika vitamkwa **i**, **a**, **u**.

Kiswahili cha Bara

- Irabu i

Kibara	Kiunguja
afriti	af <u>ir</u> iti
akdi	ak <u>id</u> i
ikrari	ik <u>ir</u> ari
rasilmali	rasilimali

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na uondoshaji wa irabu **i** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno manane, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Irabu a

Kibara	Kiunguja
barzakhi	ba <u>r</u> azakhi
wahka	wa <u>h</u> aka
zafrani	za <u>a</u> farani

Aidha kuna udondoshaji wa irabu **a** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno matano, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Zaidi ya hayo, kuna tofauti nyingine za vitamkwa zilizosababishwa na uondoshaji wa irabu katikati ya neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo.

- Irabu o

Kibara
troli

Kiunguja
toroli

- Irabu u

Kibara
wahedisitini

Kiunguja
wahediusitini

Kutokana na yaliyotangulia, tunaweza kusema kuwa udondoshaji wa irabu katikati ya neno katika Kiswahili cha Bara hutokea zaidi katika vitamkwa **i**, **a**, aidha udondoshaji wa irabu katikati ya neno hutokea zaidi kuliko mwanzoni mwa neno.

2. Udondoshaji wa Irabu mwanzoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa irabu mwanzoni mwa neno zimefikia mara 9 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Irabu i

Kiunguja
bilisi
sitiari

Kibara
ibilisi
istiara

Tunaona hapa udondoshaji wa irabu **i** mwanzoni mwa neno, nao umetokea katika maneno mawili.

Zaidi ya hayo, tofauti nyingine za aina hiyo zimetokea mara moja moja katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu a

Kiunguja
jemi

Kibara
ajemi

- Irabu u

Kiunguja
sukani

Kibara
usukani

Kutokana na yaliyotangulia hapo juu, inabainika kuwa udondoshaji wa irabu mwanzoni mwa neno katika Kiswahili cha Unguja unaweza kutokea katika vitamkwa **i , a , u**.

Kiswahili cha Bara

- Irabu **u**

Kibara	Kiunguja
bawa ⁽¹⁾	<u>ubawa</u>
hasama	<u>uhasama</u>
islamu	<u>Uislamu</u>

Hapa tunona kuwa udondoshaji wa irabu katika Kibara mwanzoni mwa neno hutokea katika kitamkwa **u** . Udondoshaji wa aina hii umetokea mara 5 katika mada ya utafiti.

3. Udondoshaji wa Irabu mwishoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno zimetokea mara 5 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

Udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno katika Kiunguja umetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu **a**

Kiunguja	Kibara
demokrasi	<u>demokrasia</u>

- Irabu **u.**

Kiunguja	Kibara
wasalam	<u>wasalamu</u>

Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno katika Kiswahili cha Unguja hutokea katika vitamkwa **a , u**

(1) Asili ya neno ni “ubawa” ila linaweza kutumika katika Kibara “bawa”. Tazama:
Kamusi ya Kiswahili Sanifu, uk. 35.

Kiswahili cha Bara

Udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno katika Kibara umetokea mara moja moja katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

- Irabu a

Kibara
asili⁽¹⁾

Kiunguja
asilia

- Irabu i

Kibara
takriban

Kiunguja
takribani

- Irabu u

Kibara
yahom

Kiunguja
yahomu

Hivyo basi, udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno katika Kiswahili cha Bara hutokea katika vitamkwa **a , i , u** .

D. Urefushaji wa Irabu:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Tanzania Bara zinaweza kusababishwa na urefushaji wa irabu katikati au mwishoni mwa neno. Tofauti za aina hii zimetokea mara 9 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Urefushaji wa Irabu katikati ya Neno

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na urefushaji wa irabu katikati ya neno zimetokea mara 6 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

(1) Ingawa aghalabu ya maneno hayo ni maneno mkopo ila hatuwezi kusema kuwa upachikaji na uondoshaji wa vitamkwa zinatokea tu katika maneno mkopo kwani kuna maneno mengine yenye asili ya Kibantu ambayo yamepatwa pia na tofauti za vitamkwa baina ya lahaja hizo mbili k.v. “dele” , “dekua” , “osha” , “pongoo” n.k.

- Irabu u

Kiunguja	Kibara
V <u>uusha</u>	vusha
Pingu <u>uso</u>	pingusi

Hapa tunaona urefushaji wa irabu **u** katikati ya neno, nao umetokea katika maneno mawili.

Aidha urefushaji wa irabu katika Kiunguja katikati ya neno umetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu a

Kiunguja	Kibara
hasha <u>akum</u> / asha <u>akum</u>	hashakum / ashakum

- Irabu i

Kiunguja	Kibara
Sabi <u>iini</u>	sabini

Hapa inabainika kuwa urefushaji wa irabu katikati ya neno katika Kiswahili cha Unguja hutokea katika vitamkwa **u , a , i** .

Kiswahili cha Bara

Urefushaji wa irabu katika Kibara katikati ya neno umetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu a

Kibara	Kiunguja
Alfa <u>aafa</u>	alfafa

- Irabu o

Kibara	Kiunguja
gook <u>a</u>	goka

Kutokana na yaliyotangulia, tunaweza kusema kuwa urefushaji wa irabu katikati ya neno katika Kiswahili cha Bara hutokea katika vitamkwa **a , o** .

2. Urefushaji wa Irabu mwishoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa zilizosababisha na urefushaji wa irabu mwishoni mwa neno zimetokea mara 3 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

Urefushaji wa irabu katika Kiunguja mwishoni mwa neno umetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Irabu i

Kiunguja
adii

Kibara
adi

- Irabu o

Kiunguja
poo!

Kibara
po!

Hapa tunaweza kuona kuwa urefushaji wa irabu mwishoni mwa neno katika Kiswahili cha Unguja hutokea katika vitamkwa **i**, **o**.

Kiswahili cha Bara

- Irabu u

Kibara
tendeguu

Kiunguja
tendegu

Hapa tunaona urefushaji wa irabu **u** mwishoni mwa neno, nao umetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia, tunaweza kusema kuwa urefushaji wa irabu katikati ya neno hutokea zaidi kuliko mwishoni mwa neno. Hali kadhalika tofauti za irabu baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Bara hutokea zaidi kuliko tofauti za konsonanti.

Sehemu ya Tatu

Tofauti za Viyeyusho

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na matumizi tofauti ya viyeyusho, navyo ni “aina ya vitamkwa ambavyo si konsonanti na wala si irabu (Nusu-Irabu); yaani ni vitamkwa ambavyo huchukuliwa kuwa viko katikati ya irabu na konsonanti. Hii ina maana kwamba kwa kiasi fulani viyeyusho hufanana na konsonanti lakini pia kwa kiasi kikubwa hufanana na irabu katika umbile la utamkaji wake”⁽¹⁾.

Matumizi tofauti ya viyeyusho yanapatikana katika upachikaji wa viyeyusho, udondoshaji wa viyeyusho, ubadilishaji wa irabu kwa viyeyusho pamoja na ubadilishaji wa konsonanti kwa viyeyusho.

A. Upachikaji wa Viyeyusho:

Tofauti za vitamkwa zilizosababishwa na upachikaji wa viyeyusho zimetokea mara 21 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Kiyeyusho y

Kiunguja	Kibara
choya	choa
chuya	chua
jiziya	jizia
nyata ⁽²⁾	nata

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa kiyeyusho y katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno manane, miiongoni mwao ni mifano ya hapo juu.

(1) Massaba & Kihore & Msanjila, uk. 28.

(2) Asili ya neni ni “nata” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “nyata”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 300.

- Kiyeyusho w

Kiunguja	Kibara
wacha	acha
winika	inika
wiva ⁽¹⁾	iva

Hapa ni tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa kiyeyusho w mwanzoni mwa neno, nayo imetokea katika maneno sita, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Kiswahili cha Bara

- Kiyeyusho w

Kibara	Kiunguja
anuwai	anuai
swahibu	sahibu

Tunaona hapa tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa kiyeyusho w katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno manne, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

- Kiyeyusho y

Kibara	Kiunguja
soroveya	sorovea
tamthiliya	tamthilia

Hapa ni tofauti ya vitamkwa inayosababishwa na upachikaji wa kiyeyusho y katikati ya neno, nayo imetokea katika maneno matatu, mionganoni mwao ni mifano ya hapo juu.

Kutokana na yaliyotangulia, inabainika kuwa upachikaji wa viyeyusho hutokea zaidi katika Kiswahili cha Unguja katika y, w . ama upachikaji wa viyeyusho katika Kiswahili cha Bara basi hutokea katika w , y . Hali kadhalika tunaweza kuona wazi kuwa upachikaji wa viyeyusho hutokea zaidi katika Kiswahili cha Unguja

B. Udondoshaji wa Viyeyusho:

(1) Asili ya maneno hayo ni: “acha”, “inika”, “iva”, ila yanaweza kutumika katika Kiunguja “wacha”, “winika”, “wiva”. Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 1, 124, 126.

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zilizosababishwa na udondoshaji wa viyeyusho zimetokea mara 6 katika mada ya utafiti kwa namna ifuatayo:

1. Udondoshaji wa Viyeyusho katikati ya Neno:

Udondoshaji wa viyeyusho katikati ya neno umetokea mara 4 kwa namna ifuatayo:

Kiswahili cha Unguja

- Kiyeyusho **y**

Kiunguja
finanga

Kibara
finyanga

Hapa tunaona udondoshaji wa kiyeyusho **y** katikati ya neno, nao umetokea katika neno moja tu.

- Kiyeyusho **w**

Kiunguja
shufa⁽¹⁾

Kibara
shufwa

Aidha kuna udondoshaji wa kiyeyusho **w** katikati ya neno, nao umetokea katika neno moja tu.

Kutokana na yaliyotangulia inabainika kuwa udondoshaji wa viyeyusho katikati ya neno katika Kiswahili cha Unguja hutokea zaidi katika vitamkwa **y**, **w**.

Kiswahili cha Bara

Udondoshaji wa viyeyusho katikati ya neno katika Kibara umetokea mara moja moja kwa namna ifuatayo:

- Kiyeyusho **w**

Kibara
uzimbezimbe

Kiunguja
uzimbwezimbwe

- Kiyeyusho **y**

(1) Asili ya neno ni “shufwa” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “shufa”.
Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 367.

Kibara
umbea

Kiunguja
umbeya

Hivyo basi udondoshaji wa viyeyusho katikati ya neno katika Kiswahili cha Bara hutokea katika vitamkwa **w**, **y**.

2. Udondoshaji wa Viyeyusho mwanzoni mwa Neno:

Kiswahili cha Bara

- Kiyeyusho **w**

Kibara
ania
aidhi

Kiunguja
wania
waidhi

Udondoshaji wa kiyeyusho **w** mwanzoni mwa neno, nao umetokea katika maneno mawili.

Hapa tunaweza kusema kuwa udondoshaji wa viyeyusho katikati ya neno hutokea zaidi kuliko mwanzoni mwa neno.

C. Mpishano wa Irabu na Viyeyusho:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na mpishano wa irabu na viyeyusho. Tofauti za aina hii zimetokea mara 8 kwa namna ifuatayo:

1. Mpishano wa Irabu na Viyeyusho mwanzoni mwa Neno:

Kiswahili cha Bara

- (**u - w**): idadi zake (2):

Kibara
welekeo
wongofu

Kiunguja
uelekeo
uongofu

2. Mpishano wa Irabu na Viyeyusho katikati ya Neno:

Kiswahili cha Unguja

- (*w - u*): idadi zake (2):

Kiunguja
suali
bueta

Kibara
swali
bweta

Kiswahili cha Bara

- (*u - w*): idadi zake (3):

Kibara
anwani
satwa

Kiunguja
anuani
satua

3. Mpishano wa Konsonanti na Viyeyusho mwanzoni mwa Neno:

Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara zinaweza kusababishwa na mpishano wa konsonanti na viyeyusho mwanzoni mwa neno. Tofauti ya aina hii imetokea mara moja tu katika mada ya utafiti:

Kiswahili cha Unguja

- (*b - w*): idadi yake (1):

Kiunguja
uwinda⁽¹⁾

Kibara
ubinda

(1) Asili ya neno ni “ubinda” ila linaweza kutumika katika Kiunguja “uwinda”.
Tazama: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, uk. 412.

Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umejaribu kutoa maoni ya awali kuhusu tofauti za vitamkwa baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Tanzania Bara. Tumeona kuwa kuna tofauti za kimsingi za vitamkwa baina ya lahaja hizi mbili. Tofauti zilizo na umuhimu zaidi ni pamoja na:

- Tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara hutokea zaidi katikati ya neno k.v. mpishano wa konsonanti, mpishano wa irabu, udondoshaji wa irabu, udondoshaji wa viyeyusho, upachikaji wa konsonanti, upachikaji wa irabu, upachikaji wa viyeyusho na urefushaji wa irabu.
- Tofauti za matumizi ya irabu baina ya Kiswahili cha Unguja na Kiswahili cha Bara hutokea zaidi kuliko tofauti za matumizi za konsonanti.
- Upachikaji wa konsonanti katikati ya neno hutokea zaidi katika Kiswahili cha Unguja.
- Upachikaji wa viyeyusho hutokea zaidi katika Kiswahili cha Unguja.

Mapendeleko

Si jambo jepesi kwamba utafiti kwa mara moja unaweza kujitosheleza na kudaiwa kuwa umemaliza kila kipengele katika eneo ulilolichunguza. Tunapendeleko kwamba vipengele zaidi vya kiisumu kuchunguzwa. Tafiti zinazopendelekezwa ni pamoja na sababu za kutokea tofauti za vitamkwa baina ya Kiunguja na Kibara.

Kiambatisho

Jedwali Na. 1: Aina za Tofauti za Vitamkwa katika Kiunguja

Aina ya Tofauti	Vitamkwa	Pahala pa kutokea zaid	Lahaja
mpishano wa konsonanti	l : r	katikati	
mpishano wa konsonanti	h : kh	mwanzoni	
upachikaji wa konsonanti	n , r	katikati	
upachikaji wa konsonanti	h , k , m	mwanzoni	
udondoshaji wa konsonanti	h	mwanzoni	
udondoshaji wa konsonanti	n	katikati	
mpishano wa irabu	e : a , e : i	katikati	
mpishano wa irabu	o : u	mwishoni	
mpishano wa irabu	e : i	mwanzoni	
upachikaji wa irabu	i	katikai	
upachikaji wa irabu	a	mwishoni	
upachikaji wa irabu	i	mwanzoni	
udondoshaji wa irabu	i , a , u	katikati	
udondoshaji wa irabu	a , u , i	mwanzoni	
udondoshaji wa irabu	a , u	mwishoni	
urefushaji wa irabu	u , a , i	katikati	
urefushaji wa irabu	i , o	mwishoni	
upachikaji wa viyeyusho	y , w		
udondoshaji wa viyeyusho	y		

Kiunguja

Jedwali Na. 2: Aina za Tofauti za Vitamkwa katika Kibara

Aina ya Tofauti	Vitamkwa	Pahala pa kutokea zaid	Lahaja
mpishano wa konsonanti	l : r , h : kh	katikati	
mpishano wa konsonanti	ch : t , l : r	Mwanzoni	
upachikaji wa konsonanti	r	Katikati	
upachikaji wa konsonanti	m	Mwanzoni	
udondoshaji wa konsonanti	h	Mwanzoni	
udondoshaji wa konsonanti	l	Katikati	
mpishano wa irabu	i : e	Katikati	
mpishano wa irabu	e : i	Mwishoni	
mpishano wa irabu	o : a	Mwanzoni	
upachikaji wa irabu	i	Katikati	
upachikaji wa irabu	u	Mwishoni	
upachikaji wa irabu	u	Mwanzoni	
udondoshaji wa irabu	i , a	Katikati	
udondoshaji wa irabu	u	Mwanzoni	
udondoshaji wa irabu	a , i , u	Mwishoni	
urefushaji wa irabu	a , o	Katikati	
urefushaji wa irabu	u	Mwishoni	
upachikaji wa viyeyusho	w , y		
udondoshaji wa viyeyusho	w, y	Katikati	
udondoshaji wa viyeyusho	w	Mwanzoni	

Kibara

Marejeo

Kipacha, Ahmad: **Launi za Kiswahili Sanifu na Kiswahili Fasaha kwa Tanzania Bara na Zanzibar, SWAHILI FORUM 19**, 2012.

BAKIZA: **Kamusi la Kiswahili Fasaha**, Oxford University Press, East African Ltd, chapa ya kwanza, 2010

Mbaabu, Ireri: **Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili**, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 2007.

Mdee, James S.: **Dictionaries and the Standardization of Spelling in Swahili**, Institute for Kiswahili Research, University of Dar es Salaam, Tanzania, <http://lexikos.journals.ac.za>

Massamba, David P. B & Y.M, Kihore & Y. P, Msanjila: **Fonolojia ya Kiswahili Sanifu**, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, chapa ya tatu, 2013, uk. 90.

Massamba, David P. B.: **Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha**, TUKI, Dar es Salaam, Tanzania, chapa ya pili, 2009.

TUKI: **Kamusi sanifu ya Isimu na Lugha**, chapa ya kwanza, Dar es Salaam, Tanzania, 1990.

TUKI: **Kamusi ya Kiswahili Sanifu**, Oxford University Press, East African Ltd, Toleo la tatu, 2014.